

# VOLUNTEER HANDBOOK

## MWONGOZO WA KUHUDUMIA SHULE ZA UMMA ZA SALEM KEIZER







**Place your school logo here**

LEARNING FOR A LIFETIME
SALEM•KEIZER
PUBLIC SCHOOLS

December 2022 HUM-F046


# Kitabu cha Maelezo

Hiki kitabu cha maelezo kimetengenezwa kusaidia wale wanaojitolea kuelewa umuhimu wa kazi wanayoifanya na kusaidia wanafunzi kuweza kufanikiwa. Kinajumuisha taarifa zinazokubalika na zisizokubalika, sera muhimu, masharti na mwongozo vinavyotakiwa kufuatwa ili kuhakikisha wanafunzi na watu wazima kwenye shule zetu wanakuwa salama. Na pia kinajibu maswali mengi yanayoulizwa wakati wa huduma ya kujitolea ...

## Faida za kujitolea kwa shule za umma za Salem-Keizer

Kuwa mtu wa kujitolea shuleni, kuna faida kwa wanafunzi, wafanyakazi, na wengine wanaojitolea. Mara nyingi wanaojitolea wamepata faida nyingi kulivyo walivyosaidia.

Kila mtu anayesaidia mtoto anaongeza mabadiliko kwenye maisha yake. Kazi inayofanywa na na watu wa kujitolea inafanya mazingira ya kusoma kuwa ya utajiri na ya maana sana



**Faida kwa WANAFUNZI:**

- Kusoma mafanikio ya kusoma kwa wanafunzi
- Kujenga kujiamini
- Kuonyesha mfano mzuri
- kuonyesha mwingiliano kwa mwanafunzi na mtu mzima anayejali
- Mwanafunzi kuangalia kwa umakini

**Faida kwa SHULE & WAFANYAKAZI:**

- Kupanua kuelewa kujifunza na ufundishaji
- Kujenga msaada wa kusaidiwa nje ya shule na elimu
- Kuongeza mawasiliano ya kuaminika kwenye jamii
- Kumsaidia mwalimu kufanya kazi na mwanafunzi kw a muda mwingi
- Kupunguza uwajibishaji

**Faida kwa WANAOJITOLEA :**

- Kupata uwelewa wa mazingira ya shule
- Kuputa uzoefu na uhusiano
- Kujenga jumuiya
- Ujuzi wa muda unaochangaia huleta tofauti!

# Watu wanaojitolea husaidia kuweka mazingira ya kusoma kwa:

- Kuzima simu unapokuwa shuleni
- Kufanya mazungumzo binafsi nje ya darasa
- Kuwa makini ya kwamba wanafunzi wanakuangalia na uwe wa mfano
- Fanyakazi kwa umakini: tafadhali usilete watoto wengine kwenye muda wa kujitolea
- Jaribu kutokuhudhuria madarasa mengine.
- Kuwa makini kwenye muda na ratiba ya wafanyakazi
- Kuvaa nguo za kikazi
- Tegemea wanafunzi wakufundishe kwa nidhamu kama unavyokuwa na nidhamu kwao.
- Waombe wanafunzi wakuite "Mr." au "Mrs." kuliko jina la kwanza.
- Fanya maamuzi mazuri.
- Fuata sera zote na utaratibu; na kama hauna uhakika wa kitu muulize mfanyakazi.

# Nani anayejitolea shuleni?


Kufuatana na Sera ya Wilaya PAP-A003 " Watu wa Kujitolea Shuleni", inatafsiriwa kama mtu binafshi ambaye siye muajiriwa wa wilaya na anayejitolea muda kuhusiana na shughuli zozote zinazohusiana na shule. Wanaojitolea hawapokei mshahara wowote isipokuwa gharama walizoingia mojamoja kwa kuombwa na uongozi wa shule.

## Mwelekeo na mafunzo

Shule za Umma za Salem-Keizer zinatoa mwelekeo na mafunzo kwa wanajiotolea wale wanaotumika kila wakati shuleni. Kwa wale wanaojitolea kwenye tukio moja kama (safari za shule) mafunzo maalumu siyo muhimu. Mwalimu wa darasa atakupa taarifa unazotakiwa. Kwenye kipindi cha mafunzo, wale wanaojitolea watapokea kwa umakini utangulizi wa sera za wilaya, matarajio na ulinzi kwa wanaojitolea, wafanyakazi na wanafunzi. Mada nyingi zinazoelezewa kwenye mafunzo, zimeelezewa kwa ufupi kwenye kitabu cha maelezo kama sehemu ya kukumbushia. Mratibu wa shule kwa wanaojitolea atakupatia ratiba iliyopo ya vipindi vya mafunzo.

## Volunteering—beginning to end

**Hatua ya kwanza ni kuangalia historia ya makosa ya jinai.** Mtu yeyote anayejitolea kwenye Shule za Umma za Salem-Keizer anatakiwa kukamilisha historia ya mchakato wa makosa ya jinai.



### Zifuatazo ni hatua:

1. **Wasiliana na shule/Mahali** utakotaka kutoa huduma ya kujitolea. Watakupatia fomu za kujaza Historia ya Makosa ya Jinai. Au, jaza fomu kwenye mtandao kupitia tuvuti ya wilaya www.salemkeizer.org. Bonyeza kwenye "wanaojitolea" kiungo kinapatikana upande wa juu kulia kwenye ukurasa.
2. **Jaza fomu** na kurudisha shuleni au moja kwa moja kwa Idara ya Mwajiri. Tafadhali hakikisha kuwa sehemu zote za fomu zimejazwa sahihi na kukamilika. Fomu isiyojazwa itarudishwa, itakataliwa au itachelewa kushughulikiwa. Kama maombi yako yatahitaji kuangaliwa zaidi, utatumiwa barua kuelezea hatua inayofuata kwenye mchakato wa kukubaliwa.
3. **Inaweza kuchukua mpaka wiki mbili kipindi cha maombi mengi ya mchakato wa historia ya makosa ya jinai**, kwa hiyo unashauriwa kujaza fomu mapema. Utasikika kutoka Idara ya Mwajiri tu kama kuna swali kuhusu maombi yako. Kuhakikisha kuwa maombi yako yamekubalika, tafadhali wasiliana na shule unayotaka kujitolea
4. **Watu wakujitolea ni lazima wakubalike na Idara ya Mwajiri KABLA ya kuanza shughuli za kujitolea.** Ili kuweka mazingira ya ufanisi na mazingira salama, uongozi wa shule unaweza kukataa mtu binafsi kujitolea katika shule pamoja na kwamba amefaulu historia ya makosa ya jinai.

Wakati wa kipindi cha shule, utafanya kazi chini ya usimamizi wa wataalamu wafanyakazi na walimu. Ni muhimu maongezi yote kati yako na wafanyakazi lazima yawe wazi, na matarajio yote yanaeleweka kwa wote wafanyakazi na wanaojitolea. Kwavile uko kwenye kundi la mazingira ya elimu, ni muhimu kuchukua majukumu ya programu kwa umakini. Wafanyakazi unaofanya nao kazi wanategemea utakuwa pale, kwahiyo itabidi kuwapa taarifa kama hautakuwepo. **Weka kumbukumbu za muda uliojitolea** katika shule au shughuli zozote nje ya siku za shule, ni muhimu. Tafadhali jiandikishe unapoingia na kutoka au kuripoti masaa yako kwa shule kama inavyotaka.

Huduma ya kujitolea ni ya mwaka mmoja wa shule. Unaweza kuanza muda wowote wa mwaka wa shule, lakini muda wa kujitolea unaisha mara shule inapokwenda mapumziko ya summer. Mahitaji ya shule yanaweza kubadilika kutoka mwaka hadi mwaka, ni muhimu kujua kwamba kuwa mtu wa kujitolea mwaka hadi mwaka kunaweza kubadilika.

Na kama unapenda kujitolea tena mwaka mwingine wa shule, huna haja ya kujaza tena historia ya makosa ya jinai (maana inatumika kwa miaka mitano na baada ya hapo itabidi ujaze tena) **Wapigie shule simu au mahali unakotaka kujitolea na waeleze ungependa kujitolea tena mwakani.** Watawasiliana na wewe muda muafaka utakapofika

## Azimio la Kuwakaribisha Salama Shuleni

Bodi ya Shule za Umma za Salem-Keizer inaelezea wilaya kujidhatiti kwa kutengeneza utamaduniwa kuwakaribisha wote. Kila mtu anakaribishwa shuleni kulingana na umri, ulemavu, mahali alikozaliwa, hatima yake ya uhamiaji, uasili, rangi, hali ya ndoa, dini, jinsia, utambuzi wa kijinsia, uwezo wa kifedha au vitu vingine. Kwa kuongezea kila mwanafunzi anahaki kupata mafanikio kwenye elimu bila kujali alikotoka au mambo mengine, na kila mwanafunzi atapewa msaada muhimu ili kuhakikisha mafanikio. Wilaya ya Salem-Keizer inatumia Lenzi ya Usawa kuhakikisha kila maamuzi yanatolewa yanakidhi mahitaji ya mwanafunzi kujumuisha kupinga ubaguzi wa rangi na kupinga kubaguliwa wale ambao wanauwakilishi mdogo. Wilaya yetu inachukua msimamo kupinga ubaguzi wa rangi na kupinga kubaguliwa wakati wakikabiliana na tabia zinazoingiliana na thamani ya upamoja kwenye usawa. Kwa taarifa zaidi angalia tuvuti ya wilaya ya Kuwakaribisha Salama Shuleni: *https://salkeiz.k12.or.us/parents/safe-welcoming/*

## Unyanyasaji na uonevu

Wilaya imejidhatiti kutoa mazingira salama na yenye ufanisi kwa wanafunzi kusoma na wafanyakazi kufanya kazi. Vitendo vya kulazimishwa, unyanyasaji, kunyanyaswa kijinsia, vitisho, kubaguliwa, kuonewa, kuonewa kwenye mitandao, na/au kuonea hatuta vivumilia. Wanaojitolea wanafanya kazi muhimu kusaidia kuweka mazingira salama. Ni muhimu sana kutoa taarifa mara moja kama unahisi mtu kuonewa au kunyanyaswa kwa uongozi wa shule au mfanyakazi wa shule. Kama inavyotakiwa na shule, ripoti zote zitakaguliwa na uongozi wa shule. Kwa tarifa zaidi na nyenzo za kujifunza zinapatikana kwenye tuvuti ya wilaya:https://salkeiz.k12.or.us/volunteering/.

## Unyanyasaji na mtoto na kutekelezwa

Kama ukatokea kuhisi mtoto ananyanyaswa wakati wa shughuli za kujitolea na wilaya, toa taarifa mara moja ya wasiwasi kwa uongozi, mshauri au mwalimu wa shule. Weka taarifa ya siri na usizungumzie mtu yeyote ile.

Kumbuka siyo kazi yako kumuuliza mtoto au kuchunguza; waachie mamlaka. Kila mtu, kujumuisha wanaojitolea wanahamasishwa kutoa taarifa wanapohisi unyanyaswaji kwa vyombo vya sheria au DHS/Child Welfare (1-855-503-SAFE (7233). Watu kwenye utaalamu kujumuisha wafanyakazi wote wa wilaya wanatakiwa kisheria kutoa taarifa kuhusu unyanyasaji wa mtoto na kutekelezwa kwa vyombo vya sheria au DHS/Child Welfare.

## Matumizi ya tumbaku, pombe na madawa ya kulevya

Matumizi ya tumbaku, bidhaa za tumbaku, zinazofanana na sigara ya kielektroniki, pombe na madawa mengine ya kulevya (Kutoa zile zilizoandikiwa na muuguzi wa afya au zile zinazopatikana juu ya kaunta) kwa wafanyakazi na kwenye majengo ya umma ya wilaya, au kwenye mali za wilaya, kujumuisha kwenye magari binafsi au ya wilaya hairuhusiwi.

## KUDUMISHA MWAFAKA WA KUJITOLEA/MKATABA & MIPAKA KWA MWANAFUNZI

MWAKA 2019, BUNGE LA OREGON LILIPITISHA NA GAVANA AKAWEKA SAHIHI KWA SHERIA YA SENATE BILL 155, ambayo inasaidia kuhakikisha usalama kwa wanafunzi wa K-12. Bunge limekataza unyanyasaji wa mtoto na vitendo vya ngono kwa wanafunzi vinavyofanywa na watu wazima ndani ya K-12, kuelezea kinachotakiwa wakati wa kutoa taarifa, na kuonyesha hatua kwa hatua shule za wilaya au wakala lazima kufuata wakati wanapotoa taarifa. Senate Bill 155 ili ongezea kuelezea vitendo vya ngono siyo tu ni vibaya vinapofanywa na wafanyakazi wa shule lakini pia wakandarasi na wakala wa Wilaya. Kama inavyooeshwa kwenye shule za wilaya za Salem-Keizer Sera ya Uongozi PAP-A001, unyanyasi wa mtoto na vitendo vya ngono kufanywa na muajiriwa wa wilaya, mkandarasi, wakala au mtu anayejitolea haitavumiliwa

SHULE ZA UMMA ZA SALEM-KEIZER ZIMEJIDHATITI kutoa mazingira ya kusoma ambayo ni huru kutoka kunyanyaswa, utovu na nidhamu na unyanywasaji. Uhusishwaji wa watu wazima kujali katika mazingira ya shule ni muhimu kwa mafanikio ya shule na usalama wa ustawi kwa wanafunzi. Hii kitabu cha maelezo ni kumkupa taarifa watu binafsi wanaojitolea, wakandarasi au watoa huduma ndani ya Wilaya kuendeleza uhusiano mzuri unaolenga kwenye mahitaji ya elimu kwa mwanafunzi na kukwepa mahusiano ambayo yanaweza kutafsiriwa vibaya.

*Kama una swali au wasiwasi tafadhali usisite kuasiliana na uongozi wa shule au mkuu wa idara au wasiliana na Debbie Joa, Mratibu wa Wilaya Kulinda na Kuzuia, kwa simu # 503-399-3061 au joa_debbie@salkeiz.k12.or.us.*

UNYANYASAJI WA WATOTO

**KURIPOTI**

If Kama umejua kuhusu unyanyasaji wa mtoto au kutelekezwa wakati unapojitolea kwenye wilaya au unawasiwasi kuhusu mwajiriwa wa wilaya, mtu anayejitolea, mkarandarasi au wakala ana mnyanyasa mtoto, toa taarifa kwa uongozi wa shule, mshauri wa shule, au piga simu Idara ya Mwajiri kwa namba 503-399-3061. Kila mtu anahamasishwa kutoa taarifa ya unyanyasaji wa mtoto kwa Oregon Department of Human Services/Child Abuse Hotline (1-855-503-7233) au kwa wakala wa vyombo vya kisheria. Watu binafsi kwenye taaluma zao kujumuisha wafanyakazi wa wilaya wanatakiwa kutoa taarifa kisheria kwa unyanyasaji wa mtoto au kutelekezwa kwa Idara ya Huduma za Jamii kwa Oregon na vyombo vya sheria.

UNYANYASAJI WA MTOTO: INAJUMUISHA KUPIGA, VITENDO VYA NGONO NA KUTUMIKA, UNYANYASAJI WA KIHISIA, KUTEKELEZWA NA KUTISHIWA KUUMIZWA..

*Kwa taarifa zaidi kuhusu kuzuia unyanyasaji wa mtoto na kutoa taarifa inapatikana Wilaya ya Shule za Salem-Keizer ukurasa wa mafunzo na wanaojitolea pamoja na wakandarasi na kwenye tuvuti ya Idara ya Huduma za Jamii kwa Oregon.*

VITENDO VYA NGONO

KAMA ILIVYOELEZEWA NA KURUDIWA KWENYE SHERIA YA OREGON YA 339.370, Vitendo vya ngono inajumuisha maneno au vitendo, maandishi au mawasiliano ya teknolojia yanayofanywa na mwajiriwa wa wilaya ya shule, mkandarasi, wakala au mtu wa kujitolea ambayo yanahusisha mwanafunzi na yanaelekeza mwendeleo wa ngono au kuomba upendeleo wa ngono kwa mwanafunzi au; mazingira ya ngono yanayoelekeza ngono kwa wanafunzi au yameathiri na kuingiliana na uwezo wa kielimu kwa mwanafunzi au umetengeneza mazingira ya vitisho na chuki.

Vitendo vya ngono havijumuishi kushikwa au kugusana kimwili ambako ni kwa lazima kwa mazingira ya kazi kwa mfanyakazi wa wilaya au huduma zinazotakiwa kutolewa na mkandarasi, wakala au mtu wa kujitolea ambapo hakuna nia ya ngono, kwa maneno, maandishi au mawasiliano ya teknolojia yanayotolewa kama sehemu ya programu inayofikia kiwango cha elimu au sera za Wilaya.

Maana ya vitendo vya ngono havitumiki kwa mwenendo au mawasiliano na wanafunzi wa sasa K-12, wanafunzi wanaofanya kazi, mkandarasi au mtu wa kujitolea kwenye Shule za Umma za Wilaya ya Salem-Keizer na makubaliano ya mahusiano na mwanafunzi mwingine wa K-12 ili mradi mahusiano haya tengenezi mazingira ya elimu ya vitisho au chuki na hayakatazwi kisheria, Sera za Wilaya au makubaliano ya ajira yeyote

“Mwanafunzi” anaelezewa kama mtu ambaye ni: wa darasa lolote kuanzia shule ya awali mpaka darasa la 12; au miaka 21 au chini na anapokea elimu au kuhusiana na huduma za elimu kwa taasisi ya elimu ambayo siyo baada ya elimu ya sekondari; au ni mtu aliyetambulika kama mwanafunzi kwa mtu aliyeshiriki vitendo vya ngono na ameondoka shule au amemaliza kutoka high skuli ndani ya siku 90 kabla ya vitendo vya ngono.

MWINGILIANO USIOFAA

## KURIPOTI

Kama umegundua kuna uwezakano wa mwenendo wa ngono au mipaka isiyofaa kwa mwajiriwa wa wilaya, mtu anayejitolea, mkandarasi au wakala kuhusiana na mwanafunzi, toa taarifa mara moja kwa uongozi wa shule, mshauri wa wanafunzi au piga simu Idara ya Mwajiri kwa Wilaya namba 503-399-3061.

MWINGILIANO UNAOFAA UNATENGENEZA MAZINGIRA SALAMA kwa wanafunzi kujifunza, kukua, kuomba msaada katika kutatua matatizo na migogoro, na kujenga ujuzi wa kijamii.

Ni muhimu kila mtu kuchukua jukumu la kuhakikisha mazingira salama na afya kwa wanafunzi. Kama umeona na kutilia shaka tabia kati ya mtu mzima na mtoto au kati ya watoto toa taarifa moja kwa moja kwa uongozi wa shule, mshauri au mwalimu wa darasa.

Mwingiliano usiofaa huvuka mipaka inayotenganisha mwanafunzi na mahitaji ya mtu mzima na kuwa watu wa lika moja badala ya kuwa mtu mzima na mtoto


- Weka mkazo kwenye mazungumko ya elimu, matukio ya shule na shughuli za shule; elekeza matatizo binafsi kwa uongozi wa shule, mshauri au mwalimu wa darasa; jizuie kutamka maoni yenye mwelekeo wa sauti ya ngono; kukwepa mazungumzo ambayo yanamfanya mwanafunzi asijisikie vizuri au kumfanya mwanafunzi kuwa msiri.
- Kaa kwenye kikundi au eneo la wazi shuleni; epuka kuwa mwenyewe na mwanafunzi.
- Wahudumie wanafunzi kwa usawa; epuka upendeleo na zawadi na kwa mwanafunzi mmoja
- Mahusiano yawe katika mazingira ya shule; usikutane na mwanafunzi nje ya shule, usimpakie mwanafunzi au kuwasiliana nawanafunzi kwa njia teknolojia (ujumbe wa maandishi, mitandao ya kijamii, kwenye michezo ya mtandaoni,n.k)
- Weka umbali binafsi na kumuangalia machoni siyo kila wakati
- Kuwa muangalifu kuhusu mgusano na mwanafunzi; kugusana inajumuisha lakini siyo tu: kupakatwa, kuchekeshwa, kukumbatiana na kusuguliwa misuli mabegani havifai.
- Hakikisha maongezi na wanafunzi yako wazi; usijihusishe na maongezi au kuingiliana na wanafunzi kwa siri au sehemu za kujificha.

*Mifano ya ziada kuhusu mwingiliano unaofaa na usiofaa unapatikana kupitia mawasiliano ya Wilaya "Kudumisha Mwingiliano Sahihi kwa Wanafunzi -Wafanyakazi"(PAP-W006) na kwenye ukurasa wa mafunzo kwa wanaojitolea na wakandarasi*

## Kutoa Dawa

Ili kusaidia kuhakikisha afya na usalama wa wanafunzi,wale wanaojitolea hawata toa dawa kwa wanafunzi. Hii inajumuisha dawa za juu ya kaunta kama vile ibuprofen au za kukohoa. Tafadhali peleka maswali yote kuhusu dawa kwa mwalimu au mfanyakazi mwingine.

## Kumruhusu mwanafunzi




Ni mfanyakazi wa shule pekee ndiyo atakaye mruhusu mwanafunzi kutoka shule. Watoto ambao ni lazima kuondoka mapema au kuna sababu yeyote lazima wapokee karatasi ya ruhusa kutoka ofisi ya shule na imewekwa sahihi kabla ya kuondoka.

## Usemi wa Kidini

Shule lazima zidumishe utengano wa kanisa na serikali kwa mujibu wa sheria ya Oregon (ORS 327.109). Hivyo basi, shule na wafanyakazi wa shule hawapaswi kuhimiza au kukatisha tamaa dini yoyote na kukuza au kuzuia dini kwa namna yoyote na mtu anayejitolea ni marufuku. Wafanyakazi wa kujitolea ambao lengo lao ni kuwashawishi au kuwaomba wanafunzi kwa mtazamo wa kidini watakataliwa kuingia shuleni wakati na muda wa masomo. Mialiko ya mikutano au matukio yanayodhaminiwa na makundi yoyote ni marufuku wakati anayejitolea yuko kwenye maeneo ya shule na wakati wa muda wa masomo, ikiwa ni pamoja na wakati wa chakula cha mchana.

## Kufungwa kwa dharura

Wanaojitolea hawatazamiwi kutoa huduma kama shule zimefungwa kwa dharura au hali mbaya ya hewa. Kama shule imefungwa kwa dharura wakati wa kutoa huduma, tafadhali fuata maelekezo ya uongozi wa jengo. Taarifa zaidi kuhusu shule kufungwa kwa dharura zinapatikanza kwenye tuvuti ya wilaya www.salemkeizer.org.

## Kuadhibiwa

Ni mara chache wanafunzi wanakuwa na shida ya tabia wakati wakiwa wako na wale wanaojitolea. Hata hivyo, wilaya ina mpango wa kuadhibu kama tukio likitokea. Jukumu la kuadhibu lipo mikononi mwa wafanyakazi; wanaojitolea hawawezi kuadhibu wanafunzi. Tafadhali mueleze mwalimu kama adhabu inatakiwa wakati unafanya kazi na wanafunzi

## Usimamizi kwa wanaojitolea

Wanaojitolea ni sehemu muhimu kwenye timu ya elimu. Ushauri na maoni yawanaojitolea yanakaribishwa siku zote. Niwafanyakazi ambao ndiyo wanajukumu kisheria kufanya maamuzi yanayofanyika kulinganana ufundishaji wa wanafunzi na usimamiziwa shule. Kwa sababu hii,wanaojitolea watafanyakazi chini ya usimamizi wa mojakwamoja wa mwalimu,uongozi nawafanyakazi wa msaada wa elimu.

Wanoajitolea na wafanyakazi mara nyingi hujenga mazingira mazuri na mahusiano ya kitaaluma. Kama kutoelewana kuna tokea, anayejitolea na mwajiriwa wanahamishwa kufanya kazi pamoja na kutatua tatizo. Ikiwa anayejitolea ana wasiwasi na mwenendo wa mfanyakazi anatakiwa kuleta matatizo yake kwa uongozi wa shule. Wilaya ina jukumu la usalama na ustawi wa wanafunzi na wafanyakazi. Kwa sababu hii, uongozi wa shule au Mratibu wa Kulinda na Kuzuia wa wilaya anaweza kumfukuka anayejitolea kama matendo yake hayana manufaa kwa shule na wanafunzi.

## Usalama kwa wanaojitolea

Wilaya inatambua kuwa kazi na mazingira yanayomzunguka anayejitolea yanaweza kuwa siyo aliyoyazoea. Wilaya itatoa mafunzo ya vifaa ili kuweza kufanya kazi salama, lakini pia wale wanaojitolea watafanyakazi baada ya kupokea mafunzo muhimu ya usalama. Kama anayejitolea ataumia wakati akiwa kwenye kazi, msimamzi na Uongozi wa hatari wanatakiwa kupewa taarifa mara moja. Wanaojitolea wana bima ya afya ya wilaya iliyokubalika kama anayejitolea atakuwa ameumia jeraha la kweli wakati akiwa atumika kwenye uwezo wa wanaojitolea wa wilaya.

Ni muhimu kwa anayejitolea kutoa taarifa ambayo siyo salama au tabia ya kibaguzi kwa mfanyakazi wa shule.

Kwenye dharura na mwongozo kuhusu moto, tetemeko la ardhi, na kufungiwa ndani ya shule, tafadhali wasiliana na shule au uongozi wa shule.

# Kanuni ya Mavazi

Nguo za heshima shuleni ni njia muhimu kuweka mazingira ya kujifunza. Wanafunzi, wafanyakazi na wanaojitolea wanategemewa kufuata kanuni ya mavazi ya shule.

Mavazi ya anayejitolea yanatakiwa kuwa ni ya kitaaluma na siyo ya kusumbua na masomo. Wilaya ina angalia kila mtazamo, ili mradi yasihamasishe vurugu, chuki, ubaguzi au kunyanyaswa. Nguo zenye maandishi kuhusu haki ya jamii zinakubaliwa; nguo zenye ujumbe wa kisiasa hauruhusiwi unapokuwa unajitolea. Ni muhimu kwa anayejitolea kuwa ni mfano kwa kuonyesha kanuni za mavazi wakati ukiwa unajitolea.

Kanuni ya mavazi inaweza kuwa tofauti katika kila shule na programu. Tafadhali ongea na ofisi ya shule au mwalimu kwa maelezo zaidi kuhusu kanuni ya mavazi.

# Kulinda usiri wa mwanafunzi

Haki ya Familia kwenye Elimu na Usiri (FERPA) ni sheria inayolinda usiri wa mwanafunzi.Wafanyakazi wa shule na wanaojitolea ni lazima kufuata kanuni za FERPA. Mfano wa taarifa zinazolindwa na FERPA inajumuisha maelezo ya kiundani kwa mwanafunzi:

- Afya, Nidhamu, Familia au hali ya makazi makazi
- Discipline
- Family or living situation
- Tabia, Utendaji kwenye masomo, Mengine
- 
- 

Ni sahihi na itagemewa kuwa wanaojiotelewa watatoa taarifa za siri walizozipata kuhusu wanafunzi kwa wafanyakazi sahihi. Isipokuwa sasa, hizo taarifa hautatakiwa kumwambia mtu yeyote nje ya shule labda tu mwalimu mkuu atakapokuruhusu kufanya hivyo.

Kuna sheria moja ambayo inaruhusu: Vitendo visivyo halali, kama kuhisi unyanyasaji wa mtoto, inatakiwa kutolewa taarifa kwa vyombo vya sheria, hata kama inamaanisha kutoa taarifa ambayo mara nyingi ilikuwa inalindwa.

Njia nzuri ya kuhakikisha unakuwa ndani ya sheria kumbuka kwamba" kilichotokea shule kinabaki shuleni" **Maana yake, taarifa za ndani kuhusu mwanafunzi ambazo umezipata wakati ukiwa unajitolea hautakiwi kushirikisha mtu yeyote lakini shule**

Hapa chini ni mifano ambayo inaweza kukupatia taarifa zinazolindwa:

- Wakati ukifundisha wanafunzi hesabu, unagundua hajifunzi kwa wepesi kama wanafunzi wengine.
- Mwanafunzi anakuambia wazazi wangu wanagombana sana na wanaweza kuachana..
- Umeshuhudia ugomvi shuleni na kujua kwamba mwanafunzi aliyeshiriki atafukuzwa.
- Wakati unasaidia darasani unajua ya kuwa mwanafunzi hasikii .
- Mwanafunzi anakuambia alama za masomo GPA.




# Kupiga picha wanafunzi

FERPA pia inawalinda wazazi na walezi kwenye haki ya kuzuia wanafunzi kupigwa picha wanapokuwa shule au wakiwa kwenye shughuli za shuleni. Zifuatato ni hatua za kufanya kabla ya kumpiga picha mwanafunzi:

5. Waulize ofisi za shule kuona kama mzazi ameruhusu mtoto wake kupigwa picha.
6. Pata ruhusa kama utabandika picha ya mwanafunzi kwenye mtandao wowote au mtandao wa kijamii, kutuma kwenye gazeti au vinginevyo kuonyesha kwenye umma. Hii ni kuhakikisha kuwa ruhusa ya kupiga picha haikukataliwa(uliza meneja wa shule kwa taarifa zaidi).
7. Hata kama kuna ruhusa imetolewa, mwanafunzi asitambulike kwenye picha(kwenye mtandao au yakuchapa) kwa jina lake lote kamili..
8. Pata ruhusa kutoka kwa mkuu wa shule kabla hujampiga mwanafunzi picha..

Tuna kushukuru wewe!

***Kazi ya wafanyakazi wa wilaya inakuzwa na watu wengi wakujitolea. Kwa niaba ya wafanyakazi wote na wanafunzi, asante kwa kuwa sehemu ya mafanikio kwa wanafunzi kwenye Shule za Umma za Salem-Keizer.Tuna thamini wewe na mchango wako kwenye shule..***